Government of **Western Australia**
Department of **Health**
**Public and Aboriginal Health Division**

# Mpango wa utoaji wa chanjo Shuleni kwa wanafunzi wenye umri wa Miaka 7 – maelezo kwa wazazi

## Chanjo ina umuhimu gani?

Chanjo hulinda watu dhidi ya magonjwa ya kuambukiza ambayo huwa na hatari kubwa ya kusababisha kuugua vibaya, ulemavu na kifo. Chanjo hutayarisha mwili kutoa kinga ambayo hulinda watu ikiwa watapata viini vya ugonjwa tena katika mazingira.

Chanjo zote zinazopatikana kwa sasa nchini Australia lazima zipite majaribio uhakiki ya usalama kabla ya kuidhinishwa. Chanjo hukaguliwa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa ni salama na zinafanya kazi ipasavyo. Dawa na chanjo zote zinaweza kuwa na athari zake. Wakati mwingine athari hizo ni mbaya sana, lakini mara nyingi athari hizo si mbaya. Ili kupata maelezo kuhusu usalama wa chanjo na athari zake za kawaida na zisizo za kawaida, tafadhali soma maelezo zaidi katika: healthywa.wa.gov/immunisation

## Mpango wa utoaji wa chanjo shuleni

Kupitia mpango huu, mtoto wako anapewa chanjo za bila malipo, zilizoratibiwa na zinazopendekezwa ili kumlinda dhidi ya:

- dondakoo, pepopunda, kifaduro – sindano 1
- virusi vya papilloma (HPV) – sindano 1.

Unaweza kusoma maelezo zaidi kuhusu magonjwa haya na chanjo zinazotumika kujikinga nayo katika: healthywa.wa.gov.au/immunisation

## Unachohitaji kufanya

Kifurushi cha idhini ya chanjo kina maelezo na fomu ya idhini.

Kama mzazi au mlezi, unahitajika:

1. kusoma kwa makini fomu ya idhini iliyoambatanishwa na karatasi ya ukweli yenye maelezo kuhusu chanjo, na utembelee healthywa.wa.gov.au/immunisation au uwasiliane na muuguzi wa shule yako ikiwa ungependa kupata maelezo zaidi
2. weka vema kwenye kisanduku chekundu au kijani katika fomu ya idhini, ili kubainisha chanjo unazozikubali, na zozote unazozikataa, kisha utie saini katika nafasi iliyotolewa
3. kutoa maelezo kwenye fomu ya idhini kuhusu matatizo ya kiafya ambayo yanaweza kuathiri mtoto wako baada ya kupokea chanjo.
4. rejesha fomu iliyojazwa shuleni, **hata kama unakataa chanjo**.

Muuguzi anaweza kuwasiliana nawe ikiwa watahitaji maelezo zaidi.

**Wanafunzi walio na fomu iliyojazwa, iliyosainiwa pekee ndio watakaochanjwa.**

Ikiwa mtoto wako hatapokea chanjo yake siku hiyo, utaarifiwa, na chaguo mbadala za chanjo zitatolewa.

## Kabla ya mtoto wako kuchanjwa

Magonjwa madogo, ya kawaida, kama vile mafua yenye viwango vya chini vya kupanda kwa joto mwilini, hayapaswi kumfanya mtoto asichanjwe. Hata hivyo katika hali zingine inashauriwa mtoto asipewe chanjo au asubiri kwa muda kutokana na hali za kiafya. Fahamisha muuguzi anayetoa chanjo au muuguzi wa shule ikiwa mtoto wako:

- amewahi kuwa na athari kali kufuatia chanjo yoyote ya hapo awali
- ana historia ya mzio mkali ambapo chanjo haipendekezwi
- amepokea chanjo ya viini hai ndani ya mwezi moja uliopita
  k.m. chanjo ya kifua kikuu, surua, homa ya manjano
- amedungwa sindano ya imunoglobulini au kuongezewa damu katika muda wa miezi mitatu iliyopita
- ana ugonjwa ambao hupunguza kinga ya mwili, (k.m. lukemia, saratani, VVU/UKIMWI) au anapokea matibabu ambayo hupunguza kinga ya mwili (k.m. dawa za steroidi kama vile hydrocortisone au prednisolone, tiba ya mionzi, tibakemikali)
- anaishi na mtu ambaye ana ugonjwa unaopunguza kinga ya mwili au anayepokea matibabu yanayopunguza kinga ya mwili
- ni mgonjwa wakati wa kupokea chanjo.

## Utunzaji baada ya kuchanjwa

Sehemu iliyodungwa sindano inaweza kuwa nyekundu na kuvimba – tumia kitambaa baridi chenye maji.

Kuna uwezekano wa kuwa na maumivu kidogo, joto jingi, maumivu ya kichwa na uchovu. Kwa maumivu ya kichwa, mpe dawa ya paracetamol kama ulivyoelekezwa kwenye lebo. Ikiwa joto haitapungua, wasiliana na daktari wako.

Tembelea healthywa.wa.gov.au/immunisation kwa maelezo zaidi kuhusu athari za kawaida na zisizo za kawiada za chanjo.

Tafuta ushauri wa kimatibabu mara moja ikiwa kuna athari ambayo unafikiri ni kali au isiyotarajiwa.

Watoa chanjo wote katika WA wanahitajika kisheria kuripoti athari mbaya baada ya kupokea chanjo. Wazazi wanaweza kuripoti pia wasiwasi kuhusu athari zozote mbaya baada ya chanjo. Pata maelezo zaidi katika healthywa.wa.gov.au/WAVSS au upige simu kwa 6456 0208.

## Rekodi za chanjo

Baada ya kuchanjwa, wanafunzi watapokea rekodi ya chanjo ambazo wamepokea.

Chanjo zote zinazotolewa kupitia mpango wa utoaji wa chanjo shuleni zimerekodiwa katika Masjala ya Chanjo ya Australia (AIR).

Unaweza kufikia Maelezo ya Historia ya Chanjo ya mtoto wako kutoka AIR ili kuhakikisha kuwa amepokea chanjo zote zilizoratibiwa kufikia sasa.

## Maelezo ya Mawasiliano

**Daktari wa eneo lako**

**Kituo cha afya cha jumuiya yako, hospitali au kitengo cha afya ya umma**
healthywa.wa.gov.au/publichealthunits

***healthdirect Australia***
Simu: 1800 022 222

## Maelezo zaidi

**Idara ya Afya**
healthywa.wa.gov.au/immunisation

**Idara ya Afya ya Jumuiya ya Madola**
1800 671 811 au
health.gov.au/health-topics/immunisation

HealthyWA
healthywa.wa.gov.au

Hati hii inaweza kupatikana katika miundo mbadala kwa kutuma ombi kwa ajili ya mtu aliye na ulemavu.

Imetolewa na Kurugenzi ya Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza
© Department of Health 2023

Hakimiliki ya nyenzo hii iko mikononi mwa Jimbo la Australia Magharibi isipokuwa kama imeonyeshwa vinginevyo. Kando na shughuli yoyote ya haki kwa madhumuni ya utafiti wa kibinafsi, utafiti, ukosoaji au uhakiki, kama inavyoruhusiwa chini ya masharti ya *Sheria ya Hakimiliki ya 1968*, hakuna sehemu ya nyenzo hii inayoweza kunakiliwa upya au kutumika tena kwa madhumuni yoyote bila idhini ya maandishi ya Jimbo la Australia Magharibi.

IMM-013031 FEB'23